

**TAARIFA YA UJENZI WA SHULE MPYA YA AWALI NA MSINGI MIVUMONI
ILIOPO KATA YA WAZO KATIKA MANISPAA YA KINONDONI.**

Shule mpya ya Msingi Mivumoni imejengwa kutokana na mahitaji makubwa ya Shule katika mtaa wa Mivumoni. Watoto wa eneo hili walikuwa wakilazimika kwenda kusoma katika Shule za msingi za **Wazo Hill, Kisauke, Benaco na Nakasangwe** ambako ni mbali zaidi ya km 3. Hivyo, Halmashauri katika kutatua tatizo hili ilitenga katika bajeti yake ya mwaka **2017/2018** kiasi cha **Shilingi 76,500,000/=** ambapo madarasa manne (4) yalijengwa na bajeti ya 2018/2019 ilitenga kiasi cha **Shilingi 131,000,000/=** kwa ajili ya ujenzi wa Shule hii. Hivyo, kufanya jumla ya fedha yote iliyotumika katika ujenzi kufikia sasa kuwa **Shilingi 207,500,000/=**.

Shule hii imejengwa katika eneo lenye ukubwa wa mita za mraba **17,555**. Aidha, Shule hii imekwisha sajiliwa na Kamishna wa Elimu kwa namba **EM.17840** mnamo tarehe **25.03.2019**.

MAENDELEO YA UJENZI:

Ujenzi wa awamu ya kwanza ulikuwa wa madarasa manne (4) yaliyoanza kujengwa tarehe **26.04.2018** na kukamilika tarehe **17.07.2018** kwa gharama ya **Shilingi 68,000,000/=**, ikiwa ni wastani wa **Shilingi 17,000,000/=** kwa kila darasa. Ujenzi wa awamu ya pili ulijumuisha madarasa matano (5), ofisi ya walimu, vyoo vya walimu matundu matatu (3), ofisi ya mwalimu mkuu na matundu kumi na tatu (13) ya vyoo vya wanafunzi pamoja na chumba maalum cha wanafunzi wa kike (Changing room).

Ujenzi huu wa awamu ya pili umegharimu **Shilingi 139,500,000/=**, ikiwa vyoo vya wanafunzi vimegharimu kiasi cha **Shilingi 29,000,000/=**, na madarasa matano (5), ofisi ya walimu, ofisi ya mwalimu mkuu na matundu matatu (3) ya vyoo vya walimu vimegharimu kiasi cha **Shilingi 110,500,000/=**. Samani za ofisi ya walimu na mwalimu mkuu zimenunuliwa kutokana na fedha hiyo.

Uwepo wa Shule hii katika Kata ya Wazo unakamilisha utekelezaji wa Sera ya Elimu ya mwaka 2014 na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 - 2020 inayotaka mwanafunzi wa Elimu ya Msingi aifikie shule ndani ya km 3. Hivyo, katika Kata hii wanafunzi wataweza kuzifikia Shule za msingi ndani ya km 3.

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa, Shule hii imejengwa kwa kutumia **force akaunti** chini ya usimamizi wa kamati na uongozi wa Shule ya msingi Wazo Hill, ambapo fedha zake zote ziliwekwa katika akaunti ya Shule ya msingi Wazo Hill.

MRADI WA UJENZI WA SHULE YA MSINGI MIVUMONI

